



## **MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA)**

### **HOTUBA YA AFISA MTENDAJI MKUU WA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA Bw. NICODEMUS D. MKAMA KATIKA HAFLA YA KUORODHESHA KWA HISA 36,613,114 ZA BENKI YA BIASHARA YA DCB KATIKA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM, TAREHE 17 MEI 2019**

---

Ndugu Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam, Ndugu Moremi Marwa,

Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Biashara ya DCB, Prof. Lucian Msambichaka;

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Ndugu Godfrey Ndalahwa;

Afisa Watendaji na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi waliohudhuria hapa;

Waandishi wa Habari;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kujumuika katika hafla hii ambayo ni ya kihistoria katika sekta ya fedha hapa nchini.

Kwa niaba ya Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), napenda kuchua fursa hii kumshukuru Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri waq Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuweza kutenga muda kutoka kwenye ratiba yake yenye majukumu mengi na makubwa ya kitaifa, na kuweza kuhudhuria hafla hii ya kuorodheshwa kwa hisa milioni 36 za Benki ya Biashara ya DCB. Kuhudhuria kwako hapa ndugu Mgeni rasmi, ni uthibitisho wa dhamira madhubuti ya serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi madhubuti wa Rais wetu Mh. Dkt John Pombe Magufuli katika kuweka mazingira bora na endelevu ya kisera, kisheria na kiutendaji yenye lengo la kukuza uwekezaji kupitia masoko ya mitaji na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla hapa nchini.

Aidha nawashukuru wageni wote waalikwa kwa kuweza kuhudhuria katika hafla hii ya kihistoria. Kuhudhuria kwenu ni uthibitisho wa nia madhubuti mliyonayo ya kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wote wa masoko ya mitaji katika kujenga masoko endelevu na yenye ufanisi, na hivyo kuchangia kujenga uchumi hapa nchini.

**Mh. Mgeni Rasmi,** Napenda kutumia fursa hii kuipongeza bodi na uongozi wa Benki ya Biashara ya DCB kwa kufanikisha zoezi la kuuza hisa kwa umma na hatimaye leo hii kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Aidha, nazipongeza Taasisi na Wataalamu wote walioshiriki katika mchakato uliowezesha benki hii kupata ridhaa ya kuuza hisa kwa umma na hatimaye leo hii kuorodhesha hisa zake katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Taasisi na wataalamu hao ni pamoja na Bodi na Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Bodi na Uongozi wa Soko la Hisa la Dar es Salaam, Mshauri kiongozi na Dalali Mfadhili wa Benki ya DCB, CORE Securities Limited, Mshauri wa Sheria, Excellent Attorneys, Mtoa Taarifa za Mahesabu, Mazars Wiscon Associates na Mawakala wa uuzaji hisa wenye leseni zilizotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana. Natambua kuwa, kazi hiyo haikuwa ndogo na rahisi lakini mmeweza kufanya kazi yenu vizuri na hivyo kufanikisha hatua hii kwa weledi na kwa ufanisi mkubwa. **Hongereni sana !!**

**Mh. Mgeni Rasmi,** Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana iliidhinisha waraka wa matarajio wa Benki ya DCB kuuza hisa za upendeleo 33,913,948 kwa bei ya shilingi 265 kwa kila hisa. Mauzo hayo yalifunguliwa mnamo tarehe 12 Novemba 2018 na kufungwa tarehe 31 Januari 2019, ambapo wanahisa wa benki

hiyo walipatiwa fursa ya kununua hisa moja (1) ya upendeleo kwa kila hisa mbili (2) walizokuwa wakizimiliki. Aidha, mauzo hayo yalitoa fursa kwa wanahisa wapya na umma kwa ujumla kununua hisa kwa bei ile ile ya hisa za upendeleo.

**Mh. Mgeni Rasmi,** Napenda kukufahamisha kuwa kupitia mauzo hayo, Benki ya DCB ilifanikiwa kuuza jumla ya hisa 36,613,114 ikilinganishwa na hisa 33,913,948 zilizotarajiwa kuuzwa, ikiwa ni sawa mauzo ya asilimia 108. Kati ya hisa zilizouzwa, hisa 23,681,321 zilinunuliwa na wanahisa wa benki ya DCB, wakati hisa 12,954,114 zilinunuliwa na wanahisa wapya wa benki hiyo.

**Mh. Mgeni Rasmi,** Mafanikio katika mauzo ya hisa za benki ya DCB yanadhihirisha imani waliyonayo wawekezaji kwa benki hii na masoko ya mitaji hapa nchini. Kupitia mauzo hayo, mtaji wa benki ya DCB unatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 16.9 na kufikia shilingi bilioni 26.7, ikiwa ni ongezeko la asilimia 57. Mafanikio haya yanaleta chachu ya maendeleo na mageuzi makubwa katika masoko ya mitaji na sekta ya fedha kwa ujumla. Aidha, Mafanikio haya ni uthibitisho kwamba wapo watanzania wengi wanaopenda kushiriki katika mfumo rasmi wa kifedha kwa kuwekeza katika masoko ya mitaji, hivyo basi jitihada zaidi zinahitajika ili kuongeza bidhaa nyingi na uwekezaji katika masoko ya mitaji hapa nchini.

**Mh. Mgeni Rasmi,** kutokana na mafanikio hayo, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imeidhinisha daftari la wanahisa wapya wa benki ya DCB, ambapo hisa zao zinatarajiwa kuorodheshwa leo hii na kuanza kuuzwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Kuorodheshwa kwa hisa za benki ya DCB pamoja na mambo mengine kunawapatia wanahisa fursa ya kuuza hisa zao endapo watahitaji kufanya hivyo na kuwezesha wawekezaji wengine kununua hisa za wale wanaouza. Hatua hii inatoa fursa kwa wataanzania wengi kushiriki katika mfumo rasmi wa kifedha kwa kuwekeza katika masoko ya mitaji hapa nchini.

**Mh. Mgeni Rasmi,** vile vile, uorodheshwaji wa kampuni katika soko la hisa la Dar es Salaam unaongeza ufanisi katika uendeshaji wa kampuni na kumwongezea mwekezaji wigo na fursa za uwekezaji. Hii inamsaidia mwekezaji kuwa na dhamana nyingi zaidi jambo ambalo hupunguza athari za uwekezaji (Risk Diversification). Pia, uwepo wa bidhaa nyingi katika masoko ya mitaji unachagua kuongezeka kwa Akiba hapa nchini; kupanuka kwa uwekezaji unaoleta ongezeko la ajira; mapato kwa njia ya kodi kwa serikali; na kuinua kipato cha wataanzia kwa ujumla.

**Mh. Mgeni rasmi,** Napenda kuhitimisha kwa kutoa rai kwa Benki na Taasisi za Fedha kutumia masoko ya mitaji ili

kuongeza kiasi cha mtaji katika taasisi zao na hatimaye kutimiza mataakwa ya kisheria ya kuwa na mtaji wa kutosha ili kuweza kujiendesha kibiashara na kuwawezesha wananchi kiuchumi na kijamii na kuweza kutoa huduma zaidi kwa wananchi hasa wanyonge walioko mijini na vijijini. Napenda kuwahakikishia kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) pamoja na wataalamu katika masoko ya mitaji wataendelea kushirikiana na wadau wote katika kutekeleza mikakati ya serikali ya kukuza na kuendeleza sekta ya fedha kupitia masoko ya mitaji endelevu, yenye ufanisi, uwazi na yenye kutoa haki sawa kwa washiriki wote, na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

**Ndugu Mgeni rasmi, wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana ahsanteni kwa kunisikiliza na ninawatakia mafanikio mema katika shughuli za uendelezaji wa uchumi hapa nchini.**